M13/2/ANSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

22132835

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI AB INITIO – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI AB INITIO – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI AB INITIO – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Friday 10 May 2013 (afternoon)
Vendredi 10 mai 2013 (après-midi)
Viernes 10 de mayo de 2013 (tarde)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.


© International Baccalaureate Organization 2013
https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU A**

# SHEREHE YA KUONJA MAEMBE: KUZA MAEMBE KUONDOA UMASIKINI

Chama cha Wakulima wa Maembe kitakuwa na sherehe ya mwaka ya kuonja maembe. Kazi mbalimbali zimepangwa katika ratiba ya sherehe hii. Siku ya kwanza ya sherehe itakuwa siku ya kuonja maembe bila kulipia. Hii itakuwa tarehe 18 Agosti. Sherehe itakuwa Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam kwa siku tano moja kwa moja kuanzia saa 2 asubuhi mpaka saa 11 jioni.

Mambo yatakayokuwa katika sherehe hii ni:

- Kuonyesha na kuonja aina mbalimbali za maembe ya kuuza na bidhaa zake.
- Kutoa maelezo muhimu kuhusu namna ya kupanda na kukuza maembe.
- Kutoa maelezo kuhusu maembe ya biashara.
- Kuwaleta pamoja watu wenye viwanda na wafanya biashara ili kupeana mawaidha.

Pia kutakuwa na mkutano kwa wote wanaohusika na kukuza maembe pamoja na biashara ya maembe.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Chama cha Wakulima wa Maembe
ambao wanapatikana kwa simu namba +255 755 252 087;
na barua pepe: mwijage@amagro.org – http://www.amagro.org

Familia, wanafunzi, wafanyabiashara, wakulima na watu wengine wote mnakaribishwa katika tamasha hili linalofanyika kila mwaka.

**KARIBUNI SANA!!!**



*What's happening in Dar es Salaam* (2010)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU B**



# TINGISHA! TINGISHA! CHEZA! IMBA! CHEZA ZAIDI!

KARIBUNI NYOTE AMBAO MMEMALIZA MITIHANI!
KARIBUNI TUTINGISHE! TUCHEZE! TUIMBE! TUCHEZE ZAIDI NA ZAIDI!

**Jumatano**

- Wanachama wa Chama cha Muziki watakutana katika Shule ya Awali ya Kimataifa ya Tanganyika (IST) kuanzia saa 1 na nusu usiku.
- Muziki utapigwa na Mac Band katika Mgahawa wa Karambezi.
- Bendi ya Roots Jazz Band itacheza katika Kilabu cha Q-Club.
- Sal Davis atatumbuiza Zanzi Club, Kempinski.

**Alhamisi**

- Muziki utachezwa katika katika Ukumbi wa *Sweet and Easy* kuanzia saa 2 usiku hadi usiku wa manane.
- Chakula cha jioni na kucheza dansi katika mgahawa wa Garden Bistro.
- Ngoma za asili, hasa Sindimba itachezwa katika Kijiji cha Makumbusho tangu mchana hadi jioni.

**Ijumaa**

- Kikundi cha Ngoma cha Kusini & Jakayo kitatumbuiza Kijiji cha Makumbusho.
- Disko la Hip Hop na Bongofleva Klabu ya Billicanas.
- Filamu ya "Sarafina" Ukumbi wa Mlimani saa 2 mpaka 6 usiku.

**Jumamosi**

- Michezo mbalimbali, pamoja na Mpira wa miguu – Chuo Kikuu Dar es Salaam tangu saa 4 asubuhi hadi jioni kabisa.
- Afro-Jazz – Karola Kinasha & Shada katika Ukumbi wa *Sweet and Easy* saa 2 mpaka 6 usiku.
- Muziki na shoo ya *Lazer* – Hoteli ya *White Sands.*
- Filamu ya *Oprah* katika Ukumbi wa *Mlimani City*.

**Jumapili**

Mapumziko

*Habari Leo Jumapili* (2011)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU C**



# MAISHA YANGU KATIKA FILAMU

Mwandishi SIMBISO MACHINE alienda kumtembelea na kumuuliza maswali Steven Kanumba, mwigizaji maarufu wa filamu nchini Tanzania, mwigizaji mchangamfu, anayependa kucheka na kutania kila wakati, anayependwa sana na vijana, na anayeweza kuigiza nafasi yoyote ile katika filamu.

SIMBISO MACHINE: **ULIANZAJE KAZI YAKO YA KUIGIZA KATIKA FILAMU?**

STEVEN KANUMBA: Tangu nilipokuwa mdogo nilipenda na nilitaka sana kuwa muigizaji. Kwa hiyo baada ya sekondari nilijiunga na vikundi mbalimbali vya kuigiza kabla ya kusoma kwa muda mfupi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhusu kuigiza.

SIMBISO MACHINE: **NA UMEPOKEA TUZO (*AWARDS*) NYINGI, SIYO?**

STEVEN KANUMBA: Ndiyo. Mwaka wa 2005 nilitangazwa kuwa mwigizaji bora wa kiume katika tuzo za Risasi. Mwaka 2006 nikapata tuzo ya mwigizaji mwenye mvuto. Mwaka 2007 nilipata tuzo ya Tanzania Vinara... na mwaka wa 2010 nilipata tuzo ya Mwigizaji Bora wa Tanzania kutoka Tuzo za Kimataifa za Hollywood John Wayne.

SIMBISO MACHINE: **HIZO NI TUZO NYINGI KWA MTU MWENYE UMRI MDOGO KAMA WEWE! UMEWAHI KUSHIRIKI KATIKA FILAMU NJE YA TANZANIA?**

STEVEN KANUMBA: Ndio, nimehusika katika filamu za Nollywood, Nigeria; na pia nimekuwa katika filamu za Uingereza na Marekani.

SIMBISO MACHINE: **UNA USHAURI GANI KWA VIJANA KUHUSU MAISHA YA SIKU HIZI?**

STEVEN KANUMBA: Vijana wasikate tamaa kuhusu maisha. Wajitahidi katika masomo yao, na wawe na malengo mazuri maishani. Waelewe kuwa chochote unachotaka kuwa, iwe ni daktari, profesa, mchumi, mwigizaji – inawezekana sana. Mradi ufanye juhudi na uweke nia thabiti ya malengo yako. Wakumbuke kuwa hata ukitaka kuruka, unaweza!

*Paa* (2010)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU D**

# MATEMBEZI MJINI NAIROBI

Kwa: bettysis@gmail.com

NORMAL

Mada: Matembezi

Mpendwa Betty,

Hujambo?

Habari za tangu wiki iliyopita? Natumai uko mzima pamoja na wazazi na ndugu zako. Mimi pia sijambo na ninaendelea vizuri na familia yangu.

Asante sana kwa kunikaribisha Nairobi na kuwa mwenyeji wangu wakati wa safari hii. Nina furaha nyingi kwa kupata nafasi ya kuja Nairobi. Nilijionea mengi yaliyonifurahisha.

Kwanza kabisa nilifurahia majengo niliyoyaona huko Nairobi. Mji wa Nairobi una majengo marefu ambayo yanayostaajabisha. Sisi huku kwetu Zanzibar hakuna majengo marefu kama hayo.

Mji wa Nairobi pia ni mkubwa sana! Nakumbuka tulivyotembea pamoja tukizuru mji huu mpaka nikachoka sana Ikabidi tukodishe teksi ya kutuzungusha. Nikilinganisha na mji wetu wa Zanzibar, ninaona mna mji mkubwa mno.

Barabara pia ni nyingi, kubwa na safi. Tena niliona bado barabara zinaendelea kujengwa. Inaonekana mji huu unaendelea kukua kwa haraka. Je miji mingine ya Kenya ina barabara kama hizi? Nina hamu ya kutembelea mji mingine ya Kenya ili nione kama kuna barabara kama za Nairobi.

Nilifurahia sana uliponipeleka mahali pa burudani. Sitasahau siku ile tulipoenda disco kule kilabu ya Carnivore. Ninakumbuka tulivyokuwa tukienda niliona mahali kwingi kwa burudani mjini Nairobi. Ninadhani kwamba watu wa mji huu wanapenda kujifurahisha sana.

Kwa kweli nilifurahia matembezi yangu ya Nairobi. Ninatarajia nitakuja tena. Asante sana.

Ni mimi rafiki yako,

Khadija

Matini asili (2012)



https://xtremepape.rs/